# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI (MB.), MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO, WAKATI AKIFUNGUA KONGAMANO LA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UTALII, KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

---

**Dodoma, Jumanne 06 Agosti 2024**

---

**Mheshimiwa Hussein Bashe (Mb.),** Waziri wa Kilimo;

**Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb.),** Waziri wa Mifugo na Uvuvi;

**Mheshimiwa Suleiman Jaffo (Mb),** Waziri wa Viwanda na Biashara;

**Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu,** Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji;

**Bwana Gerald Geofrey Mweli,** Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo;

**Prof. Riziki Shemdoe**, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

**Makatibu na Manaibu Katibu Wakuu waalikwa;**

**Waheshimiwa Mabalozi mnaowakilisha nchi zenu Tanzania;**
**Viongozi wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi;**

**Waandishi wa Habari;**

**Wageni waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana;**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

***Ndugu Washiriki***, Ninayo furaha kushirki nanyi katika Kongamano la

Uwekezaji katika sekta za utalii, kilimo, mifugo na uvuvi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya wakulima nchini, yaani Nane Nane. Ninamshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi.

***Ndugu Washiriki***, Kila mwaka, tarehe nane mwezi wa nane, nchi yetu huadhimisha siku ya wakulima. Pamoja na mambo mengine, huwa tunatumia siku hii (na wiki nzima kabla ya tarehe yenyewe) kuwashukuru wakulima kwa mchango wao mkubwa katika uhai wa Taifa letu na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Mchango wa sekta ya kilimo katika maisha na maendeleo ya nchi yetu ni dhahiri. Kwanza, kilimo ndicho kinachotupa chakula, ambayo ni hatua ya kwanza katika maisha ya binadamu. Pili, sekta ya kilimo inachangia asilimia 26 ya pato la taifa. Hii inamaanisha kuwa katika pato la taifa la shilingi trilioni 148.7 trilioni 38 zinatokana na sekta za kilimo.

Tatu, sekta ya kilimo ni chanzo na muhimili mkubwa katika ajira. Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa nguvu kazi nchini Tanzania wa mwaka 2020/2021 nguvu kazi ya Tanzania ni asilimia 54.8 ya idadi ya watu wote nchini. Hii ni sawa na watu milioni 34. Kati ya idadi hii, watu milioni 28.6 wanajishughulisha kikamilifu na shughuli za kiuchumi (economically active population), ambapo asilimia 65 wanajishughulisha na shughuli katika sekta ya kilimo (kilimo, ufugaji na uvuvi), sawa na watu milioni 18.6!

***Ndugu Washiriki***, kwa sababu nilizozieleza hapo juu, hatuna budi kwashukuru sana wakulima wa nchi hii, kwanza kwa kuendelea kulilisha taifa letu, na pili kwa kuendelea kuwa nguzo ya uchumi na maendeleo yetu kwa ujumla. Ahsanteni na Hongereni Sana Wakulima wa Tanzania!

***Ndugu Washiriki,*** katika mpango wetu wa maendeleo wa mwaka 2024/2025 tuna maeneo kumi yaliyopewa msukumo. Kwa muktadha wa kongamano hili, ninaomba niyataje maeneo matatu. Eneo la kwanza ni

kuendelea kuwekeza katika kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya mbegu bora, matumizi ya mbolea, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya zana za kisasa katika kilimo. Kama tunavyofahamu, uchumi wa viwanda tunaojaribu kuujenga malighafi zake nyingi (65%) zinategemea kilimo. Aidha, katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati, watanzania wengi wataendelea kuajiriwa na kujiajiri katika sekta ya kilimo. Hivyo, hatuwezi kuzungumzia mapinduzi ya viwanda bila kuzungumzia mapinduzi ya kilimo.

Eneo la pili ni kuchochea na kuvutia uwekezaji katika viwanda vyenye kulenga kuzalisha bidhaa zitakazoifanya nchi yetu ijitosheleze kwa mahitaji ya bidhaa muhimu nchini na kukuza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi. Kwa sasa bado zipo bidhaa ambazo tungeweza kuzizalisha hapa nchini lakini tunaagiza kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizi ni pamoja na mafuta ya kula, sukari, ngano, n.k. Aidha, mauzo yetu nje ya nchi bado yametawaliwa kwa kiasi kikubwa na bidhaa ambazo hazijaongezwa thamani.

Eneo la tatu ni kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi, hususan tukilenga kuweka mazingira maalum ya kukuza na kuimarisha biashara na uwekezaji katika sekta ya biashara ndogo na ya kati (*small and medium enterprises*). Hii ni hatua muhimu katika kurasimisha shughuli za kiuchumi nchini. Kama mnavyofahamu, sehemu kubwa ya uchumi wetu bado upo katika sekta isiyo rasmi. Kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa nguvu kazi wa mwaka 2020/2021 karibu theluthi mbili za ajira nchini zipo katika sekta isiyo rasmi. Hii inamaanisha kuwa sehemu kubwa ya uchumi hatujaweza kuiingiza katika mkondo rasmi jambo ambalo, pamoja na athari zingine, linapunguza wigo wa walipa kodi nchini.

***Ndugu Washiriki***, uwekezaji ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi wetu na katika kufikia malengo tuliyojiwekea katika mipango yetu ya maendeleo. Ili uchumi ukue kunahitajika shughuli mpya za kiuchumi. Shughuli mpya za kiuchumi maana yake ni uwekezaji mpya na kupanua uwekezaji uliopo. Ni kwa sababu hii serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeipa sekta ya uwekezaji msukumo mpya. Kwa mujibu wa takwimu za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), sekta tano zinavutia zaidi uwekezaji nchini ni ***uzalishaji viwandani***, ***usafiri na usafirishaji***, ***ujenzi wa majengo ya biashara***, ***utalii*** na ***kilimo***. Kwa kuzingatia idadi ya miradi inayosajiliwa na TIC (2021-2024), kati ya miradi 1484 iliyosajiliwa katika kipindi hiki, uzalishaji viwandani unaongoza (608, 41%), ukifuatiwa na usafiri na usafirishaji (262, 17.6%), utalii (142, 9.5%) majengo ya biashara (140, 9.4%), na kilimo (123, 8.3%). Hata hivyo, kwa kuzingatia idadi ya ajira zinazozalishwa na miradi ya uwekezaji kilimo kinaongoza. Kati ya ajira 353,133 zilizotarajiwa kuzalishwa kutokana na miradi ya uwekezaji katika kipindi tajwa jumla ya ajira 115,212 (32.7%) zilitokana na kilimo, ikifuatiwa na viwanda (95,397, 27%), usafiri na usafirishaji (39,230, 11.1%), majengo ya biashara (11,212, 3.2%) na utalii (10,266 (2.9%).

***Ndugu Washiriki,*** serikali na wadau wengine wanaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Rais wetu ameongoza mageuzi makubwa katika maeneo ya kisera na kisheria kwa kiwango ambacho jitihada hizo zimepokelewa vyema sana na jumuiya ya kimataifa. Tutaendelea na jitihada hizi. Moja ya eneo ambalo limelalamikiwa ni eneo la kodi. Kama mnavyofahamu, tayari Mheshimiwa Rais amechukua hatua za kuunda timu itakayochambua eneo na kuleta mapendekezo. Tunaamini eneo hili litapata ufumbuzi katika siku za hivi karibuni.

***Ndugu Washiriki,*** mababadiliko ya kisera na kisheria ni hatua muhimu katika kuendelea kuboresha mazingira ya biashara. Lakini hatua nyingine kubwa na muhimu ni mabadiliko katika mitazamo yetu (mindset change) juu ya biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Ni muhimu tujiulize swali la msingi: Tunapozungumzia maendeleo ya uchumi na kuondokana na umaskini wa mtu mmoja na moja, jamii na taifa na tunazunguzmia nini hasa? Au kwa maana nyingine umaskini hasa ni nini? Kwa lugha rahisi kabisa mtu anakuwa maskini

kwa kuwa hana kipato, na hivyo anakuwa hana uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu katika maisha yake. Swali la pili: mtu anapata wapi fedha? Njia ya kupata fedha ni kufanya kazi. Swali la tatu: kazi zinatoka wapi? Jibu: Biashara! Ni kweli kwamba serikali, NGOs n.k. pia zinaajiri. Lakini wote hawa wanapata fedha zao kutokana na biashara, ikiwemo kodi!

***Ndugu Washiriki,*** kwa hivyo, ni wazi kuwa kukuza biashara na uwekezaji ni njia pekee na ya uhakika ya kuleta utajiri na kuondokana na umaskini katika nchi. Na hii ndiyo tofauti ya msingi kati ya nchi maskini na nchi tajiri duniani. Hatua moja ya kupiga hatua katika maendeleo ni kuweka mazingira mazuri kwa watu kufanya biashara. Hivyo basi mtu yeyote anayekwamisha biashara na uwekezaji ni mtu hatari kwa kuwa anakwamisha jitihada zetu za kujinasua katika umaskini.

***Ndugu Washiriki,*** Hivyo basi, kupitia kongamano hili, tuendelee kutoa wito kwa sisi sote tuliokabidhiwa dhamana katika utumishi wa umma tuone kuwa moja ya jukumu letu la msingi liwe ni kusababisha biashara zitokee na zikue. Hiki kiwe ni moja ya vipimo muhimu vya ufanisi katika utendaji wetu. Tuone wakuu wetu wa mikoa na wilaya na wakurugenzi wakijivunia na kushindana kwa idadi ya biashara na uwekezaji waliosababisha kutokea na kukua katika maeneo yao ya kazi!

**Ndugu Washiriki,**

Baada ya kusema hayo, ninayo heshima sasa kutamka kuwa kongamano hili la kujadili fursa za uwekezaji katika sekta ya Utalii, Kilimo, Mifugo na Uvuvi limefunguliwa rasmi. Ninawatakia majadiliano yenye tija kwa maendeleo ya uwekezaji nchini.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**